حُسن الخلق

TABIA NJEMA

مؤلف: م عبدالملك القاسم

مترجم : الشيخ حمزة رجب سيف

محقق والمراجع: الشيخ ياسين طـه

و يونس كنون نغندا

MTUNZI: ABDULMALIK AL'QAASIM

MFASIRI NI SHEIKH. HAMZA RAJABU SEIF

KIMEREJEWA NA SHEKH: YASSINI TWAHA

NA SHEKH YUNUS KANUNI NGENDA

بسم الله الرحمن الرحيم

Utangulizi

Kila sifa njema zinamstahikia Allah Ambaye Ameumba kila kitu na akakitengeneza vizuri na kukipangilia, na akamfundisha adabu Nabii wetu Muhammad Rehma na Amani za Allah ziwe Juu Yake, kisha akazifanya kuwa ni nzuri zaidi.

Ama baada ya utangulizi huo:

Hakika Tabia njema ni sifa miongoni mwa sifa za Manabii na Wakweli na Wema, kwa Tabia hizo hupandishwa Daraja ya juu kabisa, na hupandishwa Heshima/vyeo.

Na kwa hakika Mwenyezi Mungu Mtukufu Amemuhusisha Nabii Muhammad Rehma na Amani za Allah ziwe juu yake kwa Aya ambayo imekusanya sifa zenye kusifika (na uzuri) na adabu nzuri, Akasema Mwenyezi Mungu Mtukufu: (Na hakika wewe una tabia njema).(Alqalam: 4).

Na tabia njema hupelekea kupendana na kushikamana (katika mambo ya kheri), na (kinyume chake) tabia mbaya huzaa kubughudhiana na kuhusudiana na kupeana nyongo/kupeana mgongo.

Na kwa hakika amehimiza Mtume Rehma na Amani za Allah ziwe Juu Yake, juu ya tabia nzuri na kushikamana nayo, na akaunganisha kati ya Ucha Mungu na tabia njema aliposema: (Mambo mengi yatakayo waingiza watu wengi Peponi ni kumcha Allah na kuwa na tabia njema). Hadithi imepokelewa na Imam Tirmidhi na Alhaakim).(

Na maana ya tabia njema: Ni kuuachia uso/kutabasamu, na kutoa mambo mazuri, na kujizuia kuwafanyia watu

uovu, haya ni pamoja na yale anayo shikamana nayo Muislamu katika kuongea maneno mazuri, na kujizuia na ghadhabu na kuvumilia maudhi.

Na Mtume Rehma na Amani za Allah ziwe Juu Yake alimuusia Abaa huraira Radhi za Allah ziwe juu yake usia mkubwa sana aliposema: (Ewe Abaa Huraira! Ni juu yako kushikamana na tabia njema, akauliza Abuu Huraira: na ni ipi hiyo tabia njema ewe Mtume wa Allah? Akasema: "Muunge aliyekata undugu, na umsamehe aliyekudhulumu, na umpe aliyekunyima"). Hadithi ameipokea Imam Al'baihaqi.

Na hebu zingatia kwa makini –ewe ndugu yangu mkarimu- Athari kubwa na malipo makubwa ya hili tendo zuri lililosifika, na tabia nzuri, kwa hakika amesema Mtume Rehma Na Amani za Allah ziwe Juu Yake: (Hakika mtu atafikia daraja ya Aliyefunga, na Aliyesimama usiku kwa tabia yake nzuri).Hadithi ameipokea Imamu Ahmad).(

Na hakika Mtume Rehma na Amani za Allah ziwe Juu Yake Ameihesabu tabia njema kuwa ni katika ukamilifu wa imani ya mtu Aliposema: (Mkamilifu zaidi wa imani katika waumini ni yule Mwenye tabia njema kati yao). (Hadithi ameipokea Imam Ahmad na Abuu Daud).

Na ni juu yako kushikamana na kauli ya Mtume Rehma na Amani za Allah ziwe Juu Yake: (Watu wanao pendwa zaidi na Allah ni wale wenye manufaa kati yao, na matendo yapendezayo mbele ya Mwenyezi Mungu Mtukufu, ni furaha unayo iingiza katika moyo wa Muislamu, au kumuondolea Tabu/Shida/Matatizo, au kumlipia Deni, au kumkimbizia/kumuondoshea Njaa, na kuwa sambamba/pamoja na Nduguyangu Muislamu katika shida zake inapendeza zaidi kwangu Mimi kuliko kukaa Itikafu

Msikitini Mwezi Mzima). Hadithi ameipokea Imam Twabaraaniy).(

Na Muislamu ameamrishwa kusema neno dogo laini (zuri) ili liwe hilo neno ni katika mizani ya mema yake, Amesema Mtume Rehma na Amani za Allah ziwe Juu Yake: (Na Neno zuri ni sadaka). (Hadithi imepokelewa na Imam Bukhari na Muslin).

Bali hata kutabasamu ambako hupungukiwi na chochote unapata malipo: (Na tabasamu yako mbele ya ndugu yako ni sadaka).

(Hadithi ameipokea Imam Tirmidhi).

Na maelekezo ya Mtume Rehma na Amani za Allah ziwe juu yake katika kuhimiza tabia nzuri na kuvumilia maudhi ni mengi sana na yanajulikana, na mwenendo wake ni mfano wa kufatwa katika tabia njema pamoja naye, na pamoja na wakeze, na jirani zake, na madhaifu katika Waislamu na pamoja na wajinga wao bali hata pamoja na kafiri, kwani Amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu: (Wala kuchukiana na watu kusikupeleeni kutofanya uadilifu (watu hao msiowapenda) Hivyo ndio kuwakaribu mno na ucha Mungu). (Almaaidah: 8).

Na hakika zimekusanywa alama nyingi sana za tabia njema/nzuri katika sifa nyingi, basi zitambue –ewe nduguyangu- na ushikamane nazo, kwa ufupi nikama ifuatavyo: " Ni Mtu kuwa na haya/Aibu nyingi, Maudhi machache, Mwenye kufanya Mazuri mengi, Mkweli wa Maneno, Mwenye maneno machache, Mwenye matendo mengi (ya kheri), Mwenye kuteleza kidogo, Mchache wa mambo yasiyo na faida, Mwenye kufanya wema na kuunga ujamaa/udugu, Mwenye heshima, Mwenye subira, Mwenye kushukuru, Mwenye kuridhia, Mpole, Laini, Mwenye

kujiheshimu, Mwenye huruma, si Mwenye kulaani hovyo, wala si mtusi/mwenye kutukana, wala si

m'beya/mfitinishaji,wala asiwe ni sengenyaji/kuwazungumza watu vibaya, na wala asiwe ni Mwenye pupa, wala asiwe ni Mwenye hiqdi/kinyongo, wala asiwe Bakhili/Mchoyo, wala asiwe Mwenye kuhusudu wenziwe, bali awe mkunjufu wa Uso/Moyo, Mwenye furaha kwa watu, Anapenda kwa ajili ya Allah na Anaridhia kwa ajili ya Allah na Anachukia kwa ajili ya Allah.

ASILI YA TABIA MBAYA ZOTE HUTOKANA NA: KIBURI, DHARAU/UDHAIFU NA UDHALILISHAJI. NA ASILI YA TABIA NZURI ZOTE HUTOKANA NA: UNYENYEKEVU NA HIMA YA JUU KABISA.

Ama ufakhari na kiburi/kupinga na kujiona na husda na dhulma na kujisikia na ugumu na kutakabbari/kujikweza na kupuuza na kukataa kukubali haki na kuwapendelea wengine na kutafuta ukubwa na kupenda cheo na uongozi na kusifiwa kwa yale ambayo hakuyafanya na mfano wa hayo, yote hayo yanatokana na KIBURI.

Ama uongo na dharau na khiyana na kujionyesha/riyaa na hila/udanganyifu na tamaa na kufadhaika na uogana ubakhili na kushindwa kwa jambo Fulani na uvivu na udhalili kusiko kwa Allah na kutaka kubadilisha lile ambalo ni la chini/dhalili kabisa kwa lile ambalo ni la kheri na mfano wake, hakika yote hayo yanatokana na Dharau Udhaifu na Udhalili na Udogo wa Nafsi.

SHAIRI: Utakapomtafuta Mcha Mungu utamkuta Mtu mkweli wa maneno yake na vitendo vyake

Na mtu atakapomcha Allah na akamtii, Basi mikono yake ipo baina ya mazuri na matukufu

Na kwa Mcha Mungu atakapo shikamana na Ucha MunguAna mataji mawili: taji la utulivu na taji la uzuri.

Na watakapo nasibiana watu basi sioni Nasabu inayokuwa ni nzuri kama matendo mema

EWE NDUGUYANGU MUISLAMU:

Hakika huu ni mnasaba mzuri/mtukufu wa kutaraji ujira/malipo kwa kujipamba na sifa nzuri, na kuipeleka nafsi yako kwenda kuyachukua (matendo mazuri) na kutoa juhudi katika hayo, na jihadhari juu ya kuyaacha kwa hiqdi/kinyongo na kuyachukia na kwa kusema maneno mabaya na kutofanya uadilifu na kusengenya watu na kufitinisha watu na uchoyo na kukata udugu.

Na ninashangazwa na yule aoshae uso wake mara tano kwa siku hali ya kuwa ni Mwenye kumuitikia Allah, na wala haoshi moyo hata mara moja kwa mwaka mzima ili aondoshe yale yaliyofungamana naye katika uchafu wa duniani na uweusi wa moyo(moyo mchafu) na tabia mbaya!

Na fanya pupa katika kuizoesha nafsi kuficha ghadhabu ili wafurahi walio pembeni mwako katika: wazazi wawili, mke, watoto, marafiki, na wanaojulikana/wema katika waishio nawe na kwa maneno yako matamu na ukunjufu wa sura yako na utarajie ujira/malipo katika yote hayo.

Na ni juu yako ewe nduguyangu Muislam, kushikamana na wasia wa Mtume Rehma na Amani za Allah ziwe Juu Yake uliokusanya: (Mche Allah popote ulipo, na fuatisha baya ulilofanya kwa kufanya jema, (hilo jema) litafuta hilo

baya, na changanyika/ishi na watu kwa tabia njema). (Ameipokea ImamTirmidhiy).

Alla atujaalie sisi na nyie tuwe miongoni mwa wale ambao amewasema Mtume Rehma na Amani za Allah ziwe juu yake: (Hakika atakayekuwa karibu yangu zaidi siku ya Qiyama ni yule mwenye tabia nzuri zaidi miongoni mwenu).

Ameipokea Imam Ahmad na Tirmidhiy na Ibnu Hibbaan).(

Ee Mola wetu hakika sisi twakuomba msamaha na afya usalama wa milele. Ewe Mola wetu tutengenezee tabia zetu na utupendezeshee matendo yetu, Ewe Mola wetu kama ulivyoyatengeneza vizuri maumbile yetu, basi kwa neema zako/Ihsani yako zitengeneze vizuri pia tabia zetu, Ewe Mola wetu tusamehe madhambi yetu sisi na wazazi wetu na waislamu wote. Na Rehma na Amani za Allah zimuendee nabii Muhammad pamoja na watu wa Nyumbani kwake na Maswahaba zake na Waislamu wote watakao fuata Mwenendo wake mpaka siku ya Qiyama. Aamiin!!!